

102/3

**KISWAHILI**

**FASIHI**

**KARATASI YA 3**

**JULAI/AGOSTI 2016**

**MUDA : SAA 2 ½**

**TATHMINI YA PAMOJA YA KAMDARA - 2016**

**MAAGIZO:**

- *Jibu maswali manne pekee.*
- *Swali la kwanza ni lazima.*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizosalia yaani; (Riwaya, Hadithi fupi, Tamthiliai na, fasihi simulizi).*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*
- *Sharti majibu yote yawe katika lugha ya Kiswahili*
- *Kila swali lina alama 20*

## SEHEMU YA A: USHAIRI

### 1. Swali la lazima

*Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:*

#### **ULIYATAKA MWENYEWE: D.P.B Massamba**

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,  
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo! hutaki,  
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,  
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,  
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,  
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,  
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,  
Mishikeli miamia, kwako ona haitoki,  
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,  
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,  
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,  
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,  
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,  
Ulijidhania simba, hutishiki na fataki,  
Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,  
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,  
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,  
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,  
Uliyataka mwenyewe!

Majuto ni mjukuu, huja kinyume rafiki,  
Ungejua mwisho huu, ungetenda yalo haki,  
Uko roho juujuu, popote hapakuweki,  
Uliyataka mwenyewe!

#### ***Maswali***

- a) Eleza **dhamira** ya shairi hili. (alama 2)
- b) Tambua njia **mbili** anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. (alama 2)
- c) Taja na utoe mifano ya aina zozote **mbili** za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. (alama 4)
- d) Andika ubeti wa tatu katika lugha **nathari/ tutumbi**. (alama 4)

- e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina **mbili** za idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 4)
- f) Bainisha **toni** ya shairi hili. (alama 2)
- g) Eleza **maana** ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
- (i) Mstahiki
- (ii) Hupuliki

## SEHEMU B: RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA-KEN WALIBORA

### *Jibu Swali la 2 au 3*

2. “Umenena ndipo ndugu yangu. Hiyo ndiyo tanzia ya Afrika huru.”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Ni nini sifa za mvuto zinazowaleta pamoja mzungumzaji na mzungumziwa. (alama 4)
- c) Tambua na ufafanue mbinu inayotumika katika dondoo. (alama 2)
- d) Kwa mifano mwafaka fafanua tanzia hiyo inayorejelewa katika dondoo. (alama 10)
3. Kuvunjwa kwa haki na sharia lilikuwa jambo la kawaida chini ya uongozi wa Mtemi Nasaba Bora. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea riwaya. (alama 20)

## SEHEMU C: TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA - TIMOTHY AREGE

### *Jibu swali la 4 au 5*

4. “Iwapo umefanya, yapo mengi ambayo hayakunyoka.”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Tambua mbinu moja iliyotimika katika muktadha wa dondoo. (alama 2)
- c) Fafanua kaulikwamba ‘yapomengiambayohayakunyoka’. (alama 8)
- d) Eleza jinsi baadhi ya wahusika walivyojaribu kuyanyoosha. (alama 6)
5. Kwa kutoa mifano **kumi**, eleza vizingiti walivyokumbana navyo Wanacheneo wakati wa kupigania mageuzi. (alama 20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

**DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE – K. WALIBORA NA S.A. MOHAMMED**

6. “Leo ni siku, siku ya nyani kufa ambapo miti yote huteleza”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
- c) Huku ukitoa mifano, thibitisha maudhui sita ambayo yamejitokeza katika hadithi ya Damu Nyeusi na wanayoyaendeleza. (alama 12)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

*Jibu Swali la 7 au 8*

7. (a) **Maigizo** ni nini? (alama 2)
- (b) Taja sifa **nne** za maigizo. (alama 4)
- (c) Eleza mambo **manne** anayopaswa kufanya mwigizaji ili kufanikisha uigizaji wake. (alama 8)
- (d) Ni nini **umuhimu** wa maigizo. (alama 6)
8. Kushiriki ni mbinu moja ya kukusanya data katika utafiti wa kazi za fasihi simulizi.
- a) Eleza hoja tano kuhusu umuhimu wa mbinu ya kushiriki. (alama 10)
- b) Eleza hoja tano za udhaifu wa mbinu ya kushiriki. (alama 10)